Je wanajua?

Upatikanaji wa Taarifa nchini Tanzania

Takwimu zilizowasilishwa hapa zinatoka katika vyanzo vikuu viwili. Chanzo cha kwanza ni utafiti uliohusisha maombi 131 ya wananchi ya kupatiwa taarifa kutoka idara 131 katika mamlaka 26 za serikali za mitaa, na kutoa mrejesho iwapo walipewa taarifa walizoomba. Chanzo cha pili ni utafiti wa *Sauti za Wananchi* iliyopo Twaweza, utafiti unaotumia simu za mikononi na wenye uwakilishi wa kitaifa, unaotumika kukusanya maoni ya wananchi.

Jambo la 1. Wananchi wanapoomba taarifa kutoka mamlaka za serikali za mitaa, kwenye nyakati 2 kati ya 3 hunyimwa taarifa hizo

Tulifanya utafiti katika ofisi 131 za serikali zilizopo katika wilaya 26. Maeneo yake yalichaguliwa kinasibu na kutoa uwakilishi wa kitaifa. Maafisa wa serikali walitoa taarifa zilizohitajika kwenye nyakati 1 tu kati ya tatu (33%), wakati nyakati zingine 2 kati ya 3 (67%) ya wananchi hawakupewa taarifa zozote.



Chanzo: Tanzania Mystery Shopper Survey, Twaweza na MIT GOV/LAB, 2017

Jambo la 2. Ofisi za Mipango, ardhi, na kazi ziliongoza kwa kutoa taarifa

Ofisi mbalimbali zilitembelewa katika utafiti huu zikiwemo ofisi za: Mipango, ardhi, elimu ya msingi, kazi, afya na Mkurugenzi wa Wilaya.

Ofisi za kazi, ardhi na mipango ndizo zilitoa taarifa zilizoombwa kwa kiwango kikubwa. Ofisi za Wakurugenzi wa Wilaya zilitoa taarifa kwa kiwango cha chini kabisa.



Chanzo: Tanzania Mystery Shopper Survey, Twaweza na MIT GOV/LAB, 2017

Jambo la 3. Wananchi wengi hawajawahi kusikia kuhusu taasisi muhimu za uwajibikaji kama vile Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), au Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC).

Ni mwananchi mmoja kati ya watatu (34%), aliyeshawahi kusikia kuhusu Mkaguzi Mkuu wa Serikali (CAG), na mwananchi mmoja tu kati ya sita ndiye aliyeweza kuelezea CAG ni nini. Wananchi wachache sana wanafahamu kuhusu Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC, 29%), na Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC, 26%).



Chanzo: Sauti za Wananchi, 2015

Jambo la 4. Wananchi wachache wanafahamu kuhusu sera kuu za taifa.

Mafanikio katika utekelezaji wa sera na mipango ya serikali huhitaji uelewa na ufahamu wa wananchi kuhusu sera hizo. Hata hivyo, 75% ya wananchi hawajawahi kusikia kuhusu mipango ya serikali ya mwaka 2025, na 53% hawajawahi kusikia kuhusu MKUKUTA. Sera ya Kilimo Kwanza inajulikana sana miongoni mwa wananchi japokuwa hawawezi kuelezea maana ya sera hiyo; 33% tu ya Watanzania ndiyo wanaoweza kuelezea maana ya Kilimo Kwanza.



***Chanzo**: Sauti za Wananchi, 2013*

Jambo la 5. Wananchi wachache sana wanafahamu kuhusu sheria zinazowagusa

Sheria ya Makosa ya Mtandao ilipitishwa Aprili mwaka 2015 na kuanza kutumika rasmi kuanzia Septemba mwaka 2015. Vyama vya kiraia na waandishi wa habari walionya sheria hiyo kuwa na nguvu ya kuzuia mawazo kinzani na kuchochea wadau wa vyombo vya habari na wananchi kujidhibiti wenyewe. 2% ya wananchi wanasema wanafahamu kwa kina Sheria ya Makosa ya Mtandao japokuwa 31% wameisikia tu.



Chanzo: Sauti za Wananchi, 2016

Jambo la 6. Wananchi wanaunga mkono upatikanaji wa taarifa

Wananchi wanaamini upatikanaji wa taarifa ni muhimu sana: 78% wanakubali kuwa uhuru wa kupata taarifa utasaidia kupunguza vitendo vya rushwa na maovu nchini na vilevile, 60% ya wananchi wanasema kuwa serikali izuie taarifa zile tu ambazo ni muhimu kwa usalama wa taifa.



Chanzo: Sauti za Wananchi, 2016

Jambo la 7. Wananchi wengi wangependa kupata taarifa za serikali

Idadi kubwa ya wananchi (80%) wanakubalina na kauli ya kwamba upatikanaji wa taarifa utasaidia kupambana na rushwa. Idadi kama hiyo (77%) wanasema wananchi wapate taarifa zinazomilikiwa na mamlaka za umma.

Chanzo: Sauti za Wananchi, 2015

Jambo la 8. Kiwango cha imani ya wananchi kuhusu taasisi za serikali kutoa taarifa kinatofautiana.

Wananchi wana uhakika mkubwa wa kupata taarifa kuhusu kumsajili mtoto aliyezaliwa (71%) na kuwasilisha malalamiko yao DAWASCO (63%). Kwa upande mwingine, wananchi hawana uhakika wa kupata taarifa juu ya dawa zilizokwisha (35%), ruzuku kwenye shule za msingi (39%), na mipango ya maendeleo ya wilaya na bajeti (42%).



Chanzo: Sauti za Wananchi, 2016

Jambo la 9. Wananchi wanaripoti kwamba wanapewa taarifa pale wanapoziomba

Wananchi wengi hawakuomba taarifa mara ya mwisho walipotembelea ofisi za serikali. Hata hivyo, pale walipoomba taarifa, walisema walipewa taarifa hizo. Wananchi waliripoti kuwa mamlaka za maji walijibu maombi yao yote ya taarifa walizohitaji. Matokeo haya yanaonekana kukinzana na utafiti wetu, lakini hii inaweza kusababishwa na aina tofauti ya taarifa zilizoombwa, au tofauti zilizopo kati ya taasisi zilizotembelewa.



Chanzo: Sauti za Wananchi, 2016

Jambo la 10: Wananchi 7 kati ya 10 hupata taarifa kwa kutembelea taasisi za umma

Wananchi walipoulizwa ni kwa namna gani wao hupata taarifa kutoka taasisi za umma, 74% walisema huenda kwenye taasisi husika. 14% walisema hupiga simu na 1% pekee walisema hutumia mitandao.



Chanzo: Sauti za Wananchi, 2016

Jambo la 11. Wananchi hawafahamu lini maombi yao ya taarifa yatajibiwa

12% ya wananchi wanaamini kuwa hawatapata taarifa walizoomba kutoka ofisi ya serikali. Hata hivyo, idadi kama hiyo wanaamini watapata taarifa papo hapo. Wananchi waliobaki wamegawanyika nusu kwa nusu. Kukosekana kwa sheria mahususi inayoshughulikia maombi haya huchangia wananchi kutokujua nini cha kutarajia.



Chanzo: Sauti za Wananchi, 2016